TANGAZO LA SERIKALI Na. 478 la tarehe 14/6/2024

SHERIA YA UWEKEZAJI TANZANIA,
(SURA YA 38)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 32A)*

MAREKEBISHO YA KANUNI ZA UWEKEZAJI TANZANIA YA MWAKA 2024

Jina
TS. Na.
501 la 2023

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Marekebisho ya Kanuni za Uwekezaji Tanzania za Mwaka 2024, na zitasomwa pamoja na Kanuni za Uwekezaji Tanzania za Mwaka 2023, ambazo katika Kanuni hizi zinarejewa kama "Kanuni kuu".

Nyongeza ya kanuni ya 36A

2. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kanuni ya 36 kanuni ifuatayo:

"Ushughulikiaji wa malalamiko

36A.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 32A cha Sheria, mwekezaji ambaye hakuridhishwa na mwenendo, kitendo au uamuzi wa taasisi ya Serikali kuhusu masuala ya uwekezaji, anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwenye Kituo kwa njia ya maandishi kupitia mfumo unganishi wa kielektroniki au anwani ya posta ya Kituo.

(2) Baada ya kupokea malalamiko, Kituo kitapaswa, ndani ya siku thelathini, kuitisha kikao au vikao kadiri itakavyohitajika baina ya mwekezaji na taasisi inayolalamikiwa kwa ajili ya kusikilizwa na kupata utatuzi wa malalamiko hayo.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 32A(3) cha Sheria, Kituo kinaweza, wakati wa kuchunguza na kutathmini malalamiko, kuwataka wahusika kuwasilisha nyaraka au vielelezo vyovyote vinavyohusika kwa ajili ya utatuzi wa malalamiko husika.

(4) Baada ya kuchunguza na kutathmini malalamiko ya mwekezaji chini ya kanuni ndogo ya (3), Kituo kitatoa uamuzi wake kwa njia ya maandishi na kuwasilisha uamuzi huo kwa wahusika kupitia mfumo unganishi wa kielektroniki au anwani za posta za wahusika.

(5) Endapo Kituo kitashindwa kushughulikia malalamiko ndani ya siku thelathini au mlalamikaji hakuridhishwa na uamuzi wa Kituo au namna ambavyo Kituo kimeshughulikia malalamiko hayo, mlalamikaji anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwa maandishi kwa Waziri.

(6) Baada ya kupokea malalamiko ya mwekezaji Waziri anaweza ndani ya siku kumi na nne kuthibitisha, kubadilisha au kutoa maelekezo mahsusi kuhusu uamuzi uliotolewa na Kituo.

(7) Mwekezaji ambaye hataridhika na uamuzi wa Waziri chini ya kanuni ndogo ya (6) anaweza kuendelea na taratibu nyingine za kisheria za utatuzi wa malalamiko yake.

(8) Kituo kitatunza na kuhuisha kanzidata yenye kumbukumbu za malalamiko yaliyopokelewa na kushughulikiwa na Kituo.”.

Dodoma,
23 Mei, 2024

KITILA A. MKUMBO,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,*
*Mipango na Uwekezaji*